# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 15/10/2021.

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA.

| S/N | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher J. Legonda. | Mwenyekiti |
| 2. | Albertus A. Mutabihirwa | Katibu |
| 3. | Peter A. Subadi | Mjumbe |
| 4. | Issa D. Mtweve | Mjumbe |
| 5. | Dr. Judith C. Ringia | Mjumbe |
| 6. | Maganiko B. Msabi. | Mjumbe Mshauri |
| 7. | Kwezi Kabindo | Sekretarieti |
| 8. | Marinya M. Marinya | Sekretarieti |

## WAJUMBE WASIOHUDHURIA.

1. Line E. Chanafi..............................................................................Kwa taarifa.

## AGENDA NO. 1, KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5.25 asubuhi na kuwakaribisha wajumbe wapya walioteuliwa kwa mara ya kwanza.

## AGENDA NO. 2, KUIDHINISHA AGENDA.

Katibu aliwasilisha agenda kumi na mbili kikaoni, na wajumbe wote kwa pamoja waliziidhinisha ili zijadiliwe. Agenda hizo ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuidhinisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita.
4. Yatokanayo na kikao kilichopita.
5. Kupitisha wajumbe wapya wa Bodi ya Zabuni kwenye Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Ununuzi wa Umma.
6. Kupitia taarifa ya manunuzi ya mwezi.
7. Kuidhinisha njia ya manunuzi katika ujenzi wa miradi mbali mbali iliyopo kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2021/2022.
8. Kuidhinisha manunuzi yaliyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni kupitia 'Circular Resolution'.
9. Kuidhinisha manunuzi yaliyozidi kiwango cha Mkuu wa Idara.
10. Tangazo la Zabuni ya mchujo wa awali (Pre Qualifications) kwa Mafundi Ujenzi/Wakandarasi.
11. Mengineyo.
12. Kufunga kikao.

Scanned with CamScanner

**AGENDA NO. 3 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 27/4/2021.**

Wajumbe walipitia Muhtasari na kufanya marekebisho kadha wa kadha ya uchapaji kisha kuuthibisha na kuwa kumbukumbu halali ya kikao.

**AGENDA NO.4, YATOKANAYO NA KIKAO KILICHOPITA.**

Hakukuwepo yatokanayo kwa mujibu wa kikao kilichopita lakini wajumbe waliagiza kuwa kwenye kikao kijacho cha Bodi ya Zabuni, Katibu awasilishe andiko mahususi kuhusu ukiukwaji wa taratibu za Manunuzi ya Umma unaofanywa na baadhi ya Idara katika ununuzi wa huduma ya Chakula hususani kwenye vikao vya Halmashauri pamoja na matengenezo ya magari ya Halmashauri. Katika andiko hilo wajumbe walishauri Katibu achanganue vizuri madhara yanayoweza kuipata Halmashauri kwa kukiuka taratibu za Manunuzi ya Umma.

**AGENDA NO. 5, KUPITISHA WAJUMBE WAPYA WA BODI YA ZABUNI KWENYE SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO MBALIMBALI YA UNUNUZI WA UMMA.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwajengea uwezo wajumbe wa Bodi ya Zabuni kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu utendaji kazi wao wa kila siku wa Bodi ya Zabuni. Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na uteuzi wao kwa mujibu wa Sheria, majukumu ya Bodi ya Zabuni, mamlaka ya Bodi ya Zabuni, mambo yanayoweza kusitisha uteuzi wao, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Manunuzi ya Umma, njia za Manunuzi ya Umma, Circular Resolution na matumizi yake, mamlaka za usimamizi wa Manunuzi ya Umma kwa mujibu wa Sheria, kuhitilafiana kati ya Bodi ya Zabuni na Afisa Masuhuli na kuhitilafiana katika ya Bodi ya Zabuni na PMU.

Baada ya mafunzo hayo wajumbe waliagiza katibu afanye utaratibu wa kununua vitendea kazi kama Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma ili kila mjumbe apatiwe nakala yake kuanzia kikao kijacho cha robo ya pili.

Pia wajumbe wameomba kupatiwa mafunzo ya kina ili waweze kuboresha utendaji kazi wao. Katika hilo katibu aliwahakikishia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti imetengwa kwa ajili ya mafunzo hayo.

**AGENDA NO. 6, KUPITIA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA MANUNUZI YA MWEZI.**

Scanned with CamScanner

Katibu aliwasilisha taarifa ya manunuzi ya mwezi kwa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022. Wajumbe walizijadili kwa kina na kisha waliidhinisha manunuzi hayo.

Pia katika agenda hii mjumbe mmoja alishauri 'format' ya taarifa hiyo iboreshwe ili kuongeza taarifa zinazokosekana kama kujiridhisha endapo manunuzi hayo yapo kwenye Mpango wa manunuzi.

**AGENDA NO. 7, KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI KATIKA UJENZI WA MIRADI MBALI ILIYOPO KWENYE BAJETI YA HALMASHAURI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Katibu alikieleza kikao kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 utaratibu wa kuletewa fedha za miradi ambayo ipo kwenye bajeti kuu ya Taasisi ulibadirika ambapo Taasisi hizo zitatakiwa kuandaa nyaraka za manunuzi pamoja mikataba inayoonesha gharama kwa mradi husika na kuziwasilisha Wizara ya fedha ndipo fedha zinaletwa. Moja wapo ya matakwa ya mwongozo huo ni kuitaka Bodi za Zabuni za Taasisi husika kuidhinisha matumizi ya njia ya manunuzi ya **Force Account**. Hivyo, Katibu alikiomba kikao kiidhinishe njia hiyo ili taratibu nyingine za manunuzi ziendelee na nyaraka zinazohitajika ziweze kuwasilishwa Wizarani kwa wakati.

Wajumbe kwa pamoja waliidhinisha njia hiyo ya Force account kutumika kama ilivyopendekezwa.

**AGENDA NO. 8, KUIDHINISHA MANUNUZI YALIYOIDHINISHWA NA BODI YA ZABUNI KUPITIA 'CIRCULAR RESOLUTION'.**

Manunuzi yenye thamani ya Tshs. 94,522,096.00 yaliyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni katika robo ya kwanza kwa njia ya Circular Resolution yaliidhinishwa. Pia katika agenda hii wajumbe waliagiza Katibu awe anaambatisha Circular Resolution husika zilizosainiwa kwenye taarifa hii.

**AGENDA NO. 9, KUIDHINISHA MANUNUZI YALIYOZIDI KIWANGO CHA MKUU WA IDARA.**

Agenda hii haikujadiliwa, ilishauriwa manunuzi hayo ya ufungaji wa taa za barabarani kwenye eneo la Soko la jioni yaletwe kwenye kikao kijacho yakiwa na maelezo ya kina yenye kuonyesha manunuzi hayo yatalipwa kwa njia gani na kama yapo kwenye bajeti ya Halmashauri.

Scanned with CamScanner

**AGENDA NO. 10, TANGAZO LA ZABUNI YA MCHUJO WA AWALI (PRE QUALIFICATIONS) KWA MAFUNDI UJENZI/WAKANDARASI.**

Katibu alikieleza kikao kuwa kwa mujibu wa hotuba ya Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu fedha za mgao wa UVIKO-19 ambazo nchi imepokea, katika Halmashauri yetu zitatakiwa kujenga miradi mbalimbali ya elimu. Na moja ya maelekezo yaliyotolewa ni kwamba ujenzi huo ufanywe kwa utaratibu wa Force account au Single source ambapo Local fundis na Makampuni ya ujenzi (Building Contractors) watapewa nafasi ya kutekeleza miradi hiyo. Hivyo Halmashauri inalazimika kuandaa orodha ya mafundi hao kutokana na vigezo vya awali (Pre-Qualification) ili kurahisisha matumizi ya njia hizo.

Baada ya maelezo hayo Katibu aliwasilisha tangazo hilo pamoja na njia za manunuzi pendekezwa hapo juu na wajumbe walilijadili na kisha kuliidhinisha kwa kuwa tayari walikuwa wana taarifa nalo na kutokana na uharaka wake.

**AGENDA NO. 11, MENGINEYO.**

Katika agenda hii wajumbe waliagiza Katibu awasilishe kwao makabrasha ya kikao husika mapema ili waweze kupitia makabrasha hayo mapema. Lakini hii ihusu agenda zile ambazo sio nyeti sana zenye kuhitaji usiri mkubwa.

Pia wajumbe waliagiza Katibu awe anaandaa vikao vya Bodi ya Zabuni kwa wakati.

**AGENDA NO. 12, KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio mazuri na mijadala ya kina wakati wa kikao, kisha alifunga kikao mnamo saa 8.19 mchana.

**UMEDHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ....................................... | ....................................... |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| **BODI YA ZABUNI** | **BODI YA ZABUNI.** |

Scanned with CamScanner